ONTHELINE NEWSROOMS
DEFENDING PRESS FREEDOM

# Mwongozo kwa vyombo vya habari wa kuwasaidia waandishi wanaolengwa na unyanyasaji wa mtandaoni

International Press Institute (IPI)



## *Utangulizi*

Unyanyasaji wa mtandaoni na mashambulizi dhidi ya waandishi wa habari - ikiwa ni pamoja na vitisho, matusi na kampeni za kuchafua jina - vinazidi kutumiwa kama njia ya kunyamazisha waandishi wa habari na kutia doa uaminifu wao machoni pa umma. Ingawa kushughulikia unyanyasaji wa kimtandao na athari zake mbaya kwenye mtiririko mkubwa wa habari kunahitaji kuhusisha watu wengi, vyumba vya habari vina jukumu muhimu katika kuwalinda waandishi wao kutokana na madhara ya kitaaluma na binafsi ambayo unyanyasaji unaweza kusababisha. Muongozo huu unaelezea hatua mahsusi ambazo vyumba vya habari vinaweza kuchukua.

Hatua zilizomo kwenye Itifaki hii zinatokana na taarifa zilizokusanywa na IPI wakati wa ziara za ana kwa ana kwenye vyumba vya habari 45 katika nchi tano za Ulaya - Finland, Ujerumani, Poland, Uhispania na Uingereza - kati ya Aprili na Desemba 2018 pamoja na mikutano na wataalamu kutoka nchi mbalimbali. Kwa ujumla, IPI ilihoji wahariri, waandishi wa habari na wawakilishi kutoka asasi za kiraia zaidi ya 110 pamoja na wataalamu wa sheria, wawakilishi wa asasi za kiraia na wanazuoni. Kama sehemu ya ziara hizo ndani ya nchi husika, jumla ya vikundi vya majadiliano nane vilivyohusisha waandishi wa habari wanawake na waandishi wa habari wa kujitegemea vilifanyika kujadili athari za unyanyasaji wa kimtandao kwa makundi hayo hasa.

Muongozo huu, ambao umechapishwa kama sehemu ya programu ya IPI ya Newsrooms Ontheline, haukusudiwi kuwa maelekezo yanayoweza kutatua matatizo yote kila mahala bali kama sehemu ya kuanzia kwa viongozi wa vyumba vya habari kuwasaidia kubuni mfumo unaofaa zaidi kwa mazingira yao na ambao unaweza kudumishwa kwa muda mrefu.

# *Yaliyomo*

**Hatua ya 1: Kutoa Taarifa** 3

a. Tengeneza utamaduni wa usalama katika chumba cha habari kuhusiana na unyanyasaji wa mtandaoni
b. Weka njia na hatua za wazi za kutoa taarifa za unyanyasaji
c. Hifadhi kumbukumbu za matukio ya mashambulizi na unyanyasaji wa mtandaoni

**Hatua ya 2: Kutathmini hatari** 5

a. Hatari ya madhara ya kimwili
b. Hatari ya madhara ya kisaikolojia
c. Hatari ya madhara ya hadhi

**Hatua ya 3: Mifumo ya msaada** 7

a. Msaada wa usalama wa kidijitali
b. Msaada wa kisheria
c. Msaada wa kihisia na kisaikolojia
d. Likizo ya muda mfupi, kuhama na/au kupewa majukumu mengine
e. Taarifa kwa umma ya msaada
f. Kudhibiti unyanyasaji wa mtandaoni

**Hatua ya 4: Kufuatilia na kutathmini upya** 12

**Majukumu na kazi** 13

- Mratibu wa Usalama wa Mtandaoni
- Wasimamizi
- Wahariri
- Waongozaji
- Waandishi wa habari

# Hatua ya 1: Kutoa taarifa

## a Tengeneza utamaduni wa usalama katika chumba cha habari kuhusiana na unyanyasaji wa mtandaoni

*Uongozi unapaswa kuchukua hatua zote zinazohitajika kuelewa aina za mashambulizi ambazo wafanyakazi wao na wachangiaji wanakabiliana nazo na kufanya mazungumzo kuhusu mashambulizi hayo kuwa ni ya kawaida.*

- ***Memorandamu ya ndani***: Tuma barua pepe kwa wafanyakazi wote ikieleza wazi kuwa shirika la habari linachukulia mashambulizi ya mtandaoni kwa uzito mkubwa. Hatua hii ni muhimu kujenga imani katika chumba cha habari. Inatoa ujumbe muhimu mbili: Kwanza, inasaidia kukanusha hisia zilizosambaa miongoni mwa waandishi wa habari kwamba kulengwa na matusi kwenye mitandao ya kijamii ni hali mpya na ya kawaida; na pili, inawapa wanahabari hisia za usalama kwamba shirika la habari litawaunga mkono.

- ***Zungumza mara kwa mara kuhusu unyanyasaji wa mtandaoni katika mikutano ya kazi***: Namna moja kwa wahariri kuzungumzia suala hili ni kwa kuuliza tu kama kuna waandishi wa habari ambao walengwa hivi karibuni pamoja na kukuza uelewa kuhusu hatari ya mashambulizi wakati wa kugawa kazi ambazo zinaweza kusababisha unyanyasaji. Wakati wa mgogoro wa kisiasa au machafuko ya kijamii au kabla ya uchaguzi, mazungumzo haya yanapaswa kuwa ya mara kwa mara.

- ***Sambaza** **utafiti wa siri*** ndani ya chumba cha habari ili kuangalia athari za unyanyasaji wa mtandaoni na ufanisi wa hatua zilizowekwa kukabiliana nao.

> *Tovuti ya habari za mtandaoni ya Kihispania Publico.es ilifanya utafiti wa wafanyakazi wake ili kutathmini athari za unyanyasaji kwa wafanyakazi wake pamoja na ufanisi wa hatua ilizoweka.*

- ***Anzisha mikutano ya mara kwa mara kati ya timu za mitandao ya kijamii na wanahabari*** ili kufanya ***"ukaguzi wa afya"*** unaohusiana na kazi za waandishi wa habari kwenye mitandao ya kijamii au ushiriki katika sehemu za maoni mtandaoni

- ***Tengeneza** **sehemu rahisi kufikika*** ndani ya mtandao wa ndani wa chombo cha habari iliyo na taarifa kuhusu sera za kampuni juu ya unyanyasaji wa kimtandao na nyenzo na mwongozo ambazo kampuni imetengeneza kushughulika na tatizo hilo.

> *Katika mtandao wake wa ndani, BBC ina filamu za kielimu ambapo waandishi wa habari wanajadili msongo wa mawazo wakiwa kazini na athari zake kwao. Filamu hizo hufanya kazi kama aina ya "mwongozo wa mwanzo" juu ya msongo wa mawazo na kusaidia kufafanua suala hilo.*

## b Weka njia na hatua wazi za kutoa taarifa

*Wafanyakazi wote na wachangiaji wanapaswa kujua wanapaswa kutoa taarifa za unyanyasaji kwa nani na kwa jinsi gani. Vyumba vya habari vinapaswa kuunda njia mbalimbali ambazo kupitia hizo mashambulizi yanaweza kuripotiwa kwa urahisi na kuruhusu wanahabari kupata msaada.*

### *Njia zisizo rasmi za kutoa taarifa:*

- ***Himiza** **mazungumzo yasiyo rasmi** **miongoni mwa wafanyakazi***: Vyumba vya habari vinapaswa kuwahimiza wanahabari kubadilishana uzoefu wa unyanyasaji miongoni mwao wenyewe na wahariri wao. Inapaswa kufafanuliwa wazi kwamba kuzungumza wazi kuhusu mashambulizi ya mtandaoni si dalili ya udhaifu au unyonge.

- ***Tengeneza** **grupu la mazungumzo*** kwa njia ya Whatsapp, Messenger majukwaa mengine kama hayo (Signal, Telegram, nk.) ambapo waandishi wa Habari wanaweza wakasema juu ya unyanyasaji wanaokutana nao mtandaoni. Mazungumzo ya kawaida tu yanaweza kuongeza uelewa juu ya swala hili pamoja na kujenga hali ya mshikamano.

### *Njia rasmi za kutoa taarifa:*

- ***Tengeneza** **fomu ya mtandaoni*** mahali ambapo mwanahabari aliyelengwa na mashambulizi ya mtandaoni anaweza kutoa taarifa kwa

urahisi. Fomu hii inapaswa kuwa fupi na rahisi kujaza, lakini ikigusia taarifa zote za muhimu kuhusiana na shambulizi.

- *Tengeneza* ***anauani maalumu ya barua pepe*** ambapo wanahabari wanaweza kutoa taarifa juu ya unyanyasaji wa mtandaoni.

Mifumo rasmi ya kutoa taarifa inatengeneza matarajio ya kuchukuliwa kwa hatua. Hivyo ni lazima ikawekwa wazi kwa waandishi wa Habari, wafanyakazi wengine, na wachangiaji ambao wana wajibu wa kupokea taarifa hizo na hatua hizi mtu huyo anaweza kuchukua. Mtu huyu lazima awe anafahamu kuhusu suala la unyanyasaji (ni vyema akawa amepokea mafunzo) na awe na hadhi ya kuweza kulipeleka swala hili katika ngazi za juu katika shirika ambazo zinaweza kutoa majibu au kuchukua hatua.

Bila kujali ikiwa tukio limeamuliwa kupelekwa ngazi za juu au la, wale wanaoripoti wanapaswa kupokea aina fulani ya majibu ili kufanya iwe wazi kwamba ripoti zao zinasikilizwa na kudumisha uaminifu katika mfumo huo. Hatimaye, kwa kuzingatia kwamba wanawake na makundi maalumu wanakuwa waathirika zaidi wa unyanyasaji, vyumba vya habari vinapaswa kuhakikisha kwamba waratibu wa mifumo ya kuripoti wanajumuisha wawakilishi kutoka makundi haya na/au wamepewa uelewa wa aina maalum za mashambulizi yanayolenga wanawake na makundi maalumu

## C Tunza kumbukumbu ya matukio ya mashambulizi ya mtandaoni na unyanyasaji

Hii maana yake ni kwamba kwa upande mmoja, waandishi wa habari wanaoshambuliwa wanapaswa kutunza picha (screenshots) za mashambulizi na kunakili taarifa zingine zinazohusiana. Utunzaji mzuri wa kumbukumbu ni muhimu katika kuelewa vyanzo vya mashambulizi, kufanya uhakiki wa hatari na kuamua hatua gani chombo cha Habari kinapaswa kutekeleza. Kwasababu ya ukubwa wa mashambulio fulani, wanahabari wanapaswa kutiwa moyo kuwachagua wenzao, wahariri au viongozi wengine katika mchakato wa kutunza taarifa ili kujipunguzia mzigo.

Kwa upande mwingine, wale walio na wajibu wa kuratibu mfumo wa kutoa taarifa wanapaswa kutengeneza **kanzidata ya kufuatilia matukio ya unyanyasaji wa mtandaoni** yaliyoripotiwa kwao na taarifa juu ya hatua zilizochukuliwa. Kanzidata hii ni muhimu katika kufuatilia hatua za msaada zilizotolewa na ufanisi wake (angalia taarifa zaidi katika Hatua ya 4).

# Hatua la 2: Kutathmini hatari

Tathmini ya hatari ya kina ni muhimu ili kuamua ni aina gani ya msaada inafaa zaidi panapotokea shambulio ya mtandaoni. Aina za hatari zifuatazo zinapaswa kufanyiwa tathmini:

- Uwezekano kwamba ***shambulio la mtandaoni likageuka kuwa shambulio la mwili***.
- ***Uwezekano wa madhara ya kihisia*** kwa mwandishi aliyelengwa na madhara katika kazi yake.
- Uwezekano wa kampeni ya kuchafuana mtandaoni ***kuharibu hadhi na heshima/uaminifu*** wa mwanahabari na/au chombo cha habari.

Wale wanaohusika na kufanya tathmini hii wapatiwe mafunzo ya kutosha yatakayo wawezesha kutambua uwepo wa vigezo fulani na kuelewa wakati gani wa kulipeleka tukio husika katika ngazi za juu. Hapa chini kuna baadhi ya sababu zinazoweza kutumika kutathmini kiwango cha hatari. Mchakato wa kutathmini hatari unapaswa pia kuhusisha walengwa wa mashambulizi.

## a Hatari ya madhara ya kimwili

***Mambo ya kuzingatia:***

- Mazingira ya kiusalama kwa ujumla (wingi wa mashambulizi ya mwili dhidi ya waandishi, kutokuchukuliwa kwa hatua zozote dhidi ya mashambulizi hayo, mazingira ya kuenezwa kwa chuki kwa ujumla dhidi ya waandishi na vyombo vya habari).
- Katika tukio la mshambuliaji mmoja, tathmini ya hatari ya shambulio la mwili kutokana na taarifa zinazojulikana kuhusiana na mtu huyu.
- Katika tukio la kampeni, uwezekano kwamba mtu zaidi ya mmoja watalengwa au kuhalalishwa kufanyiwa shambulio la mwili.
- Ukaribu kwa umma wa kazi za mwandishi: Anaweza kutambulika kwa urahisi kiasi gani katika maeneo ya umma?

## b Hatari ya kuumizwa kisaikolojia

*Mambo ya kuzingatia:*

*Viashiria vya nje:*

- Uzito/ukubwa wa unyanyasaji, kwa maudhui na marudio (unyanyasaji wa "kiwango cha chini" unaojirudiarudia unaweza kusababisha madhara).
- Uwepo wa maudhui ya kibaguzi (kuhusu jinsia, rangi, utambulisho wa kingono nk.), ambayo yanawezakuwa na madhara kwa mlengwa.
- Uwepo wa picha za kutisha.
- Jumbe zinazoonyesha tabia za kumfatilia mtu kupindukia, ambazo zinaweza kujenga hofu na hali ya kujisikia kutokuwa salama.
- Uimara wa mfumo mzima wa msaada kwa mlengwa.
- Viashiria vya ndani:
- Hali ya kisaikolojia ya mlengwa: Dalili za msongo wa mawazo.

## c Hatari ya kuvunjiwa heshima

***Mambo ya kuzingatia:***

- Kiwango cha chuki kilichopo katika jamii dhidi ya chombo cha habari.
- Uwezekano wa uzushi kuaminiwa na umma.
- Kiasi na usambaaji wa mashambulizi na kampeni chafu, ikiwa ni pamoja na sababu/mambo ambayo yanaweza kuruhusu mashambulizi ya mtandaoni kusambaa kwa haraka zaidi kama vile:
  - Matumizi ya memes au vibonzo vingine vilivyobuniwa.
  - Matumizi ya kurasa za mitandao bandia .
  - Matumizi ya majina mabaya yaliyo na uwezekano wa kutumika tena siku za usoni.
  - Usambazwaji zaidi wa mashambulizi kupitia tofuti za habari potofu.
  - Dalili kwamba kampeni chafu zimetengenezwa kwa niaba ya maslahi ya kisiasa, kiuchumi au mengine.

Sababu hapo juu si pekee. Inashauriwa kwamba vyumba vya habari viwekeze katika mafunzo ya taaluma ili viweze kung’amua hatari za kimwili, msongo wa kihisia, na hatari ya kuumizwa ki-hadhi, ikiwa ni pamoja na ishara za kampeni chafu zinazo ratibiwa.

# Hatua ya 3: Kutekeleza Mifumo ya Msaada

Sehemu hii inatoa muhtasari wa mifumo ya msaada inayoweza kuanzishwa pale mwandishi anapolengwa na mashambulio ya mtandaoni au unyanyasaji. Dhumuni la mifumo yote hii ni kuhakikisha kwamba waandishi wanaolengwa wanaweza kufanya kazi zao kwa.

## a Msaada wa usalama wa kidijitali

***Hii inaweza kuwa pamoja na***, *kwa mfano:*

- ***Kuwafatilia wanaofanya mashambulizi***, hata kama wanawezakuwa wametuma vitisho kupitia akaunti za mitandao ya kijamii zisizo na majina halisi.
- ***Kufunga akaunti zote za mlengwa***, kubadilisha nywila, nk., ili kupunguza hatari.
- Mhariri na wanahabari wenza waombe kuzichukua akaunti za mitandao ya kijamii za mlengwa ili kwamba asiendelee kushambuliwa zaidi.

*Hatua za kuzuia:*

- ***Wajulishe wanahabari juu ya taarifa binafsi*** zinazopatikana kwa umma kupitia mitandao ya kimajii. Angalia kama kuna taarifa zozote nyeti zimewekwa hadharani bila idhini.
- ***Wafunze waandishi wa habari kukagua vifaa vyao vya kielektroniki*** kutambua ikiwa kuna udhaifu ambao wadukuzi wanawezza kuutumia kupata taarifa zao binafsi na kuzisambaza hadharani.

## b Msaada wa kisheria

*Uamuzi wa ikiwa hatua ya kisheria ichukuliwe ama la dhidi ya unyanyasaji wa mtandaoni unapaswa kuchukuliwa ukizingatia mambo kadhaa.* ***Pamoja na:***

- Ikiwa chapisho lina maudhui yaliyo kinyume cha sheria kulingana na sheria zenu
- Uwezekano kwamba kufungua kesi kutawatisha washambuliaji wengine kwa ujumla siku za usoni
- Uwezekano kwamba kufungua kesi kutazuia vitendo vya mshambuliaji husika katika kesi
- Uwezekano kwamba, kwa kuzingatia mazingira husika, kuchukua hatua za kisheria kutaweka mwangaza kwa mwandishi husika na kuongeza na kuhamasisha mashambulizi zaidi
- Kama hatua za kisheria bila kukusudia zinaweza kupigia muhuri hoja ambazo washambulizi wa mtandaoni tayari wanaweza kuwa wanasambaza kuhusu vyombo vya habari "yenye nguvu" kushambulia "mtu mdogo", na hivyo kusababisha unyanyasaji zaidi.
- Kama shambulio linaonekana kuwa limetekelezwa na mtu binafsi anayefanya peke yake au kushiriki katika kampeni iliyoratibiwa. Katika hali ya pili, hatua za kisheria zinaweza kuwa na matokeo yasiyofaa na kuchochea mashambulizi zaidi.
- Matokeo yanayowezekana kwa mwandishi husika; Je, kesi itamridhisha au itamuumiza kihisia zaidi mwandishi anayeshambuliwa?
- Ikiwa waendesha mashitaka wameichukua pia kesi hiyo, kitu ambacho inawezakuwa rahisi zaidi kuunga mkono juhudi hizo

**MSAADA ZAIDI**: Tovuti ya IPI Newsrooms Ontheline ina **mfululizo wa video** zinazofundisha mambo gani ya kuzingatia unapoamua **kufungua mashtaka ya kisheria**.

## c Msaada wa kihisia na kisaikolojia

*Msaada wa kisaikolojia wa kitaalamu*

Msaada wa kitaalamu wa afya ya akili unaweza kuwa na jukumu muhimu katika kusaidia kupunguza athari za unyanyasaji wa mtandaoni na unyanyasaji wa wanahabari. Kama utaratibu bora, vyombo vya habari vinapaswa kuhakikisha kwamba waandishi wa habari wanapata huduma za afya ya akili kupitia mpango wa afya wa shirika au kupitia mipango ya dharura iliyofanywa kati ya chombo cha habari na wataalamu wa afya ya akili.

### *Msaada miongoni mwa waandishi*

Kwa wanahabari wanaolengwa na unyanyasaji wa mtandaoni, wenzao ambao wamepitia masaibu kama hayo wanaweza kuwa msaada muhimu kutiana moyo na kubadilishana maarifa kuhusu jinsi ya kukabiliana vyema na mashambulizi na uwezekano wa athari zake

- ***Mtandao rasmi wa msaada miongoni mwa wanahabari:*** Tengeneza mtandao rasmi wa wafanyakazi ndani ya chumba cha habari ambao wako tayari kusikiliza uzoefu wa wenzao waliolengwa na unyanyasaji wa mtandaoni na kuwasaidia kupitia njia za kukabiliana na athari zake. Kwa kawaida, wafanyakazi wanaoshiriki katika mipango hii wanapaswa kuwa na mafunzo maalum juu ya jinsi ya kufanya tathmini ya msongo wa mawazo kupitia mazungumzo rasmi na waweze kuwaelekeza wanahabari kwa wahusika muhimu ndani ya chumba cha habari ambao wanaweza kuwapatia msaada wa kiafya, pamoja na aina nyingine za msaada kama ushauri wa kisheria, usimamizi wa hadhira, usalama wa kidijitali au mbinu nyingine za usalama.

  > *Pitia uchambuzi wa kina wa mtandao wa wafanyakazi wenza wa Dart Center na utekelezaji wake pale Shirika la Utangazaji la Australia*
  >
  > *Pitia mtandao wa msaada wa wafanyakazi wenza wa BBC*
  >
  > *Pitia mtandao wa msaada wa wafanyakazi wenza wa Reuters*

- ***Programu za ushauri:*** Mpe mwanahabari mwandamizi jukumu la kuwafunza waandishi wachanga. Walezi wanapaswa kuwasaidia wale wanaolelewa kutambua unyanyasaji mtandaoni, mada ambazo mara nyingi husababisha, na mitindo ambazo zinaweza kuchukua

- ***Kikundi cha mazungumzo*** cha WhatsApp, Messenger au programu kama hiyo inaweza kutumika sio tu kuripoti vitisho lakini pia kutoa usaidizi katika kesi ya shambulio.

- ***Mazungumzo ya kawaida:*** Wahariri wanapaswa kuhimizwa kutengeneza fursa za kujadili suala la unyanyasaji mtandaoni katika mtindo wa kikundi. Mifano inawezakuwa ni pamoja na:
  - “Mazungumzo wakati wa kahawa” ambapo wanahabari kutoka chumba cha habari au vyombo vingine vya habari huelezea uzoefu wao wa kukabiliana na unyanyasaji wa mtandaoni wakiwa wanakunywa kahawa. Mazungumzo haya ya “wataalamu kwa uzoefu” yanaweza kuleta elimu ya muhimu na msaada zaidi katika “kuvunja ukimya” linapokuja suala la kujadili unyanyasaji wa mtandaoni kwa uwazi.
  - Kuvunja nguvu ya unyanyasaji wa mtandaoni kupitia ucheshi. Kwa mfano, walengwa wa mashambulizi wanaweza kuona kama wangependa kuweka ukutani maoni wanayopokea mitandaoni. Kuyasoma maoni hayo kwa sauti pamoja na wenzao na kuyacheka kunaweza kuwa na athari mbaya. Vyumba vya habari vimeripoti kwamba hatua kama hizo zinaweza kusaidia kupunguza wasiwasi na mvutano na nyakati zingine kusaidia kuweka mashambulio katika mtazamo mzuri.

### *Mpango wa kujitunza kwa wanahabari*

Zaidi ya hatua zinazotolewa na vyumba vya habari na mashirika mengine, waandishi wa habari wanapaswa kuhimizwa kuunda mpango wa kujitunza ili kupunguza hatari ya msongo wa mawazo wa muda mrefu unaotokana na unyanyasaji mkali wa mtandaoni.

> **MSAADA ZAIDI:** Tovuti ya IPI ya Newsrooms Ontheline inayo  mfululizo wa video jinsi ya kukabiliana na unyanyasaji.

## d Likizo ya muda mfupi, kuhama eneo na/au kupangiwa kazi nyingine

Kulingana na tathmini ya msongo wa mawazo wa mwandishi aliyeathiriwa, likizo fupi ya muda inaweza kupunguza athari za msongo huo. Kutoa likizo katika hali kama hizi ni jambo la kawaida katika vyumba vya habari, hasa katika idara zinazokumbana mara kwa mara na maudhui yenye vurugu au yenye msongo mkubwa kama vile idara zinazoshughulikia maudhui yanayozalishwa na watumiaji (UGC).

*Gazeti la KiFini Turun Sanomat lilimuhamisha mmoja wa wanahabari wake kutoka jiji la Turku (takribani watu 250,000) na kumpeleka katika jiji la Helsinki lenye watu wengi baada ya mfululizo wa vitisho vya mtandaoni vilivyofuatiwa na vitisho vya moja kwa moja vya mtaani. Katika jiji kubwa, uwezekano wa kujulikana ulikuwa mdogo zaidi.*

## e Tamko la umma la msaada

Kwa chombo cha habari, ***kuonyesha uungaji mkono hadharani*** kwa mwandishi anayeshambuliwa kutoa au kutotoa tamko la umma la msaada kunatoa ujumbe kwamba shirika linasimama nyuma ya wafanyakazi wake na linaona mashambulizi dhidi ya waandishi wake kama shambulio dhidi ya taasisi nzima. Hata hivyo, inategemea na tukio husika, inaweza kuwa bora kutokuzungumza sana ili kuepuka kumtangaza sana mwandishi na hivyo kuhamasisha mashambulizi zaidi. Vigezo vifuatavyo vinapaswa kutumiwa wakati wa kuzingatia:

- Itakuza shambulio?
- Itasababisha unyanyasaji zaidi?
- Itakuwa na madhara yoyote kwenye kesi ambayo shirika linafikiria kufungua?

## f Kuongoza unyanyasaji wa mtanndaoni

*Mkakati wa **kina na ulioboreshwa vizuri wa kudhibiti maoni ya watumiaji** ni muhimu ili kuhakikisha kwamba mashambulizi yanayowalenga waandishi wa habari na mashirika ya habari yanaondolewa haraka, pamoja na maoni mengine yasiyokubalika.*

### *Kuzuia unyanyasaji wa mtandaoni*

- *Tengeneza **Miongozo ya Jamii** au **sera za matumizi ya mtandao***, ambazo ni zana muhimu kwa watumiaji na wasimamizi. Miongozo hii ya ushiriki itafafanua kwamba ukosoaji unakaribishwa lakini matusi, mashambulizi, chuki na vitisho havitavumiliwa.

  *Soma **Viwango vya jamii vya Guardian** na miongozo ya ushiriki.*

  *Soma **sera ya matumzi mazuri ya mtandao ya Deutsche Welle***

- ***Jenga Jamii:*** Japo inachukua muda kujenga na kuendeleza jamii ya mtandaoni, hizi ni za muhimu sana linapokuja swala la kupamba na unyanyasaji wa mtandaoni. Wasomaji wanaohisi kuwa sehemu ya jamii wana uwezekano mkubwa wa kutetea shirika la habari au mwanahabari anayelengwa na matusi au kutishiwa kwenye mitandao ya kijamii na sehemu za maoni za vyombo vya habari.
- *Anzisha **mpango wa usajili** kwenye chombo **chako cha habari:*** Ni utaratibu mzuri kuwaomba watumiaji wajisajili ili waweze kutoa maoni. Sharti hili ni muhimu sio tu kwa kuzingatia majukumu ya kisheria yanayoweza kutokea, bali pia kama kizuizi cha awali ili kuwazuia washambuliaji na akaunti zinazoendeshwa na mashine.
- ***Ruhusu maoni** katika baadhi ya maudhui:* Ikiwa hakuna rasilimali za kutosha kuongoza maoni, mbinu bora ni kufungua sehemu ya maoni kwa baadhi ya maudhui pekee. Kwa kufanya hivyo, chagua baadhi ya mada kuhakikisha kwamba jamii yako ina uwezekano wa kutoa maoni yao kwa mada mbali mbali.
- ***Zuia maoni** kwa wakati fulani:* Iwapo unahofia kutoweza kudhibiti mijadala usiku kucha au wakati wa mwisho wa wiki au wakati mwingine wowote ambapo wasimamizi hawawezi kujitolea muda wa kutosha kwa kazi hiyo, fikiria kuzuia uwezekano wa kutoa maoni kwa kipindi husika cha muda. Ukifanya hivyo, hakikisha watumiaji wako wanafahamishwa ni lini wataweza kutoa maoni tena.
- ***Dhibiti muda wa** maoni:* Mbinu nyingine ya kuwapa watumiaji fursa ya kutoa maoni huku ukipunguza mzigo kwa timu yako ni kuruhusu maoni kwa muda mfupi tu baada ya makala kuchapishwa
- ***Weka kengele ya kukukumbusha matumizi ya watumiaji wako:*** Mara nyingine, mazungumzo ambayo yamekuwa kimya kwa muda fulani yanaweza kufufuka tena ghafla. Ikiwa hutaki kufunga sehemu za maoni, tumia mfumo wa kutoa taarifa ambao utawajulisha wasimamazi wa maoni mabadiliko haya

### *Kusimamia na kujibu unyanyasaji wa mtandaoni*

Kumbuka kwamba kuondoa mashambulizi, vitisho, na matusi yanayowalenga wanahabari hakupunguzi hatari ya shambulio la kimwili kutoka kwa mshambuliaji. Wasimamizi wanaoona ujumbe wa mashambulizi unaomlenga mwanahabari, hasa ujumbe ule wenye vitisho, wanapaswa sio tu kuondoa ujumbe huo bali pia kuwafahamisha watu husika katika shirika la habari, ikiwa ni pamoja na mlengwa wa shambulio hilo

***Maoni katika Wavuti:***

- ***Kuondoa** kwa maoni:* Maoni yanayojumuisha vitisho, matusi au mashambulizi mengine dhidi ya mwandishi yanahitaji kuchunguzwa kwa karibu na wasimamizi, ambao watapaswa kuamua kama maoni hayo yanakubalika kama ukosoaji halali na/au yanakiuka Miongozo ya Jamii na hivyo kuhitaji kuondolewa. Uamuzi wowote kuhusu kuondoa maoni yanayoshambulia mwandishi unapaswa kuzingatia sio tu maudhui ya shambulio bali pia hatari inayomkabili mwandishi. Ni vyema kutoa taarifa kwa watumiaji kuhusu sababu za kuondolewa kwa maoni yao na ni vifungu vipi vya Miongozo yako ya Jamii vilivyovunjwa na maoni hayo.
- ***Onyo na kuwazuia** watumiaji:*
    - ***Wape onyo watumiaji wanaovunja Miongozo ya Jamii mara kwa mara:*** Njia nzuri ya kuonya watumiaji wanaovunja Miongozo ya Jamii mara kwa mara ni kuzuia uwezo wao wa kutoa maoni kwa kipindi cha muda. Kila wakati unapochukua hatua hii, hakikisha watumiaji wanapokea ujumbe kutoka kwako unaeleza kwa nini uamuzi huu umechukuliwa.
    - ***Wajulishe watumiaji pale akaunti zao zinakuwa zimefutwa:*** Kuondoa kabisa upatikanaji wa maoni kwa mtumiaji ni hatua kubwa na jibu sahihi kwa mashambulizi makubwa. Watumiaji ambao akaunti zao zimeondolewa wanapaswa kupokea ujumbe unaeleza sababu zilizopelekea uamuzi huo.
- ***Ushiriki wa wasimamizi** katika mazungumzo ya watumiaji:* Wasimamizi wanapaswa kushiriki katika mazungumzo kupitia akaunti ya chombo cha habari na kuwaonya watumiaji kuhusu kanuni zilizomo katika Miongozo ya Jamii. Ushiriki wa waandishi wa habari katika mazungumzo unaweza kuboresha ubora wa mazungumzo lakini haupaswi kulazimishwa, na hatari zake zinapaswa kuzingatiwa kwa makini.

***Katika majukwaa ya mitandao ya kijamii:***

Mashirika ya vyombo vya habari hutumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kufikia hadhira pana, kuchagiza mijadala ya umma kuhusu masuala fulani na, hatimaye, kuunda jamii. Vyombo vya habari vinaelekea kutumia viwango sawa vya jamii kwenye mitandao yao rasmi ya kijamii kama wanavyofanya kwenye majukwaa yao ya majadiliano, ambapo timu za wasimamizi hushirikiana na hadhira na kuunda mfumo wa mijadala ya umma yenye afya pamoja na/ na miongoni mwa watumiaji.

***Kudhibiti unyanyasaji wa kimtandao Facebook:***

- ***Futa maoni*** yakiwa na maudhui ya uchokozi na/au vitisho au maneno ya dhihaka na matusi. Hata hivyo, ukosoaji, bila kujali jinsi ulivyo mkali, unapaswa kuruhusiwa.
- ***Ficha maoni*** yenye maudhui ya kunyanyasa. Wasimamizi kwa ujumla huona hii kuwa na ufanisi mdogo ikilinganishwa na kuondoa kabisa maudhui kwa sababu mtumiaji na marafiki wa mtumiaji bado wanaweza kuona maudhui husika, hata kama wengine hawawezi.
- ***Mpige marufuku mtumiaji katika ukurasa wa Facebook wa chombo cha Habari*** wakati mtumiaji ameweka maoni ya chuki au matusi mara kwa mara, hata baada ya kuonywa. Hii inafanywa ili kuondoa mtumiaji anayeonekana kudhoofisha mara kwa mara thamani ya mijadala ya wazi.
- ***Muondoe mtumiaji kwenye ukurasa***, kama onyo la kuzuia maoni zaidi ya matusi. Ina athari ndogo kuliko kuzuia kabisa kwani mtumiaji anaweza 'ku-like' au 'ku-follow' ukurasa tena.
- ***Zima/zuia sehemu ya maoni***, ingawa kipengele hiki kinapatikana tu kwenye machapisho ya video. Hii inafanywa wakati timu ya usimamizi haina rasilimali za kudhibiti mtiririko wa maoni kwenye video au matangazo ya moja kwa moja.
- ***Zuia maneno*** na ongeza nguvu ya chujio la maneno yaliyo na ukakasi.
- 

- **Toa taarifa kuhusu chapisho au Ukurasa** ambao umevunja viwango vya jamii vya Facebook na vile vya chombo cha habari.

***Kudhibiti unyanyasaji wa kimtandao Twitter:***

- ***Kuzima:*** Linapokuja suala la unyanyasaji wa mtandaoni unaovunja viwango vya jamii vya chombo cha habari na vile vya Twitter, wasimamizi huamua kunyamazisha akaunti badala ya kuzizuia. Chaguo hili hupunguza athari za moja kwa moja za unyanyasaji lakini pia huzuia uwezekano wa hasira kwani mtumiaji aliyenyamazishwa hana habari kuhusu kunyamazishwa kwake. Hatimaye, kunyamazisha kunawawezesha wasimamizi kuona maudhui yanayotolewa katika akaunti zilizonyamazishwa na hivyo kubaki macho kwa vitisho vyovyote vinavyoweza kuwa vya uhakika

- ***Kuzuia:*** Wasimamizi huwa wanazuia akaunti zinazotuma maudhui yasiyo na maana mara kwa mara au udanganyifu, vinginevyo wasimamizi kwa ujumla hupitisha hatua hii kama hatua ya mwisho kabisa ili kuepuka hasira kutoka kwa akaunti zilizozuiwa kwa vile watumiaji wanajulishwa wanapozuiwa. Pia, kwa vile msimamizi hatakuwa na uwezo wa kufikia akaunti iliyozuiwa, inafanya iwe vigumu kufuatilia tishio lolote la haraka.

- ***Kuripoti:*** Wasimamizi huripoti twiti au akaunti kwa Twitter ambazo zinasambaza vitisho vya kuaminika na vinavyoweza kutokea au maudhui yaliyo na picha za kutisha au zenye ukatili.

- ***Kuziba majibu:*** Wasimamizi wanaweza kuficha majibu kwenye twiti zao. Watumiaji wote bado wanaweza kufikia majibu yaliyofichwa kupitia kitufe cha jibu lililofichwa, ambayo inaonekana kwenye twiti ya mwanzo kabisa wakati kuna majibu yaliyofichwa. Hata hivyo, Twitter ilihimiza uwezo huu wa kufika majibu kwa nia ya kupunguza athari za unyanyasaji au maoni ya matusi ili yasitawale mazungumzo. Msimamizi anapoficha jibu, mwandishi wa jibu hatapokea taarifa

# Hatua ya 4: Kufuatilia na Kutathmini Upya

*Vyumba vya habari vinapaswa kufuatilia matukio yaliyoripotiwa ya unyanyasaji wa mtandaoni na kutathmini upya mifumo ya usalama na msaada ili kuwalinda waandishi wa habari dhidi ya unyanyasaji wa mtandaoni.*

Mashirika ya habari **yanapaswa kutengeneza kanzidata** kufuatilia matukio ya unyanyasaji wa mtandaoni na hatua zilizochukuliwa. Kanzidata hii haihitaji kujumuisha kila tukio la unyanyasaji, lakini inapaswa kujumuisha angalau matukio yaliyoripotiwa na wafanyakazi kupitia mifumo rasmi ya kuripoti au pale ambapo tathmini ya hatari imepelekea utekelezaji wa hatua za msaada.

Madhumuni ya msingi ya hifadhidata hii ni kufuatilia matukio yaliyoripotiwa ya unyanyasaji wa mtandaoni na kuruhusu tathmini ya mara kwa mara ya hatua za msaada zilizotekelezwa, ikiwa ni pamoja na kama hatua mpya au tofauti zinahitajika.

Mbali na kutathmini hatua za msaada zenyewe, vyumba vya habari vinapaswa pia kutathmini upya mara kwa mara ufanisi wa miundo yao ya jumla ya kukabiliana na unyanyasaji. Hii inapaswa kujumuisha tafiti za ubora ili kupima kiwango ambacho wafanyakazi na wachangiaji wanahisi suala hili linachukuliwa kwa umakini pamoja na mapitio ya idadi ya matukio ambapo aina fulani ya hatua zilichukuliwa.

# Wadhifa na majukumu

***Haya ni maelezo ya wadhifa na majukumu*** *yanayohitaji kuzingatiwa. Katika vyumba vya habari vidogo, baadhi ya majukumu haya yanaweza kufanywa na mtu mmoja tu.*

### *Mratibu wa Usalama wa Mtandaoni*

Wasifu huu unajumuisha mfululizo wa kazi ambazo zinaweza kugawanywa kwa uwazi miongoni mwa wafanyakazi au kupewa mtu maalum:

- Kuwa kama mtu ambaye wanahabari wanaweza kumjulisha juu ya matukio ya unyanyasaji wa mtandaoni.
- Kushirikiana na waandishi wa habari walengwa, mhariri na mkuu wa wasikilizaji kutathmini kila kesi ya unyanyasaji wa mtandaoni na kupendekeza mifumo ya msaada ambayo mwanahabari anayelengwa anahitaji.
- Pale inapohitajika, shirikiana na uongozi na wataalamu wa sheria katika kuchukua hatua ya kitaasisi kutoka kwa chombo cha habari.
- Weka kumbukumbu za kesi za unyanyasaji wa mtandaoni zikiwa zimesasishwa ili kufuatilia na kutathmini ufanisi wa hatua zilizotekelezwa.
- Kutokana na mabadiliko ya aina ya mashambulizi ya mtandaoni, pitia mara kwa mara hatua ambazo chumba cha habari kimeweka ili kuzuia na kujibu unyanyasaji wa mtandaoni
- Kuwa kama kituo cha uratibu na elimu kwa hatua hizi. Mratibu wa Usalama wa Mtandaoni anapaswa kuwa na ufahamu wa kina kuhusu hatua zote za chumba cha habari, aweze kuzifafanua kwa waandishi wa habari wanaokabiliana na unyanyasaji wa mtandaoni na awe mtu wa kwanza kwa utekelezaji.
- Hudhuria mikutano ya kujadili habari mara kwa mara ili ufahamu aina ya habari ambazo zinaweza kuibua unyanyasaji wa mtandaoni.

### *Uongozi*

- Tambua kwamba unyanyasaji wa mtandaoni ni tatizo kubwa na kwamba shambulio dhidi ya mfanyakazi mmoja ni shambulio dhidi ya shirika lote la habari. Wasilisha msimamo huu mara kwa mara kwa chumba cha habari.
- Fanya mabadiliko ya kimuundo katika chumba cha habari ili kutengeneza mazingira mazuri ambayo kutoa taarifa juu ya unyanyasaji wa mtandaoni hakupokelewi kwa unyanyapaa. Hakikisha kwamba rasilimali za kutosha, muda na ufadhiri unawekwa ili kuimarisha miundo hii mipya.

Teua mtu mmoja au zaidi kuwa Mratibu wa Usalama Mtandaoni, kama ilivyoelezewa hapo juu.

- Wajumuishe walengwa wa mashambulizi ya mtandaoni katika michakato ya maamuzi inayowaathiri

### *Wahariri*

- Tambua kwamba unyanyasaji wa mtandaoni ni suala kubwa na lisilokubalika na si tabia tu ya uandishi wa habari wa kisasa.
- Mara kwa mara zungumzia unyanyasaji wa mtandaoni kama mada katika mikutano ya uhariri. Kuzungumza waziwazi kuhusu suala hili kutaunda mazingira ambapo waandishi wa habari watahisi vizuri zaidi kuripoti mashambulizi.

### *Wasimamizi*

- Tambua vitisho vya mtu binafsi na kampeni zilizopangwa kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii na sehemu za maoni zinazowalenga wafanyakazi, viweke kwenye kanzidata na uvisambaze kwa mwandishi wa habari, mhariri, na mtaalamu wa usalama wa mtandaoni.
- Changia katika tathmini ya kiwango cha tishio la unyanyasaji wa mtandaoni.
- Chukua akaunti za mitandao ya kijamii za mwandishi wa habari anayelengwa ili kupunguza athari yake kwa maudhui ya vurugu na kupunguza uwezekano wa msongo wa mawazo

### *Wanahabari*

- Elewa kwamba unyanyasaji wa mtanndaoni ni jambo kubwa na halikubaliki na sit u mtindo wa uandishi wa kisasa.
- Shiriki katika fursa zote za mafunzo zinazotole-

wa na chombo cha habari, ikiwa ni pamoja na uhamasishaji, usalama wa kidijitali, na udhibiti wa hatari ya msongo wa mawazo.

- Shiriki katika fursa za misaada ya wenyewe kwa wenyewe iliyo rasmi na isiyo rasmi.
- Toa taarifa ya masuala ya unyanyasaji wa mtandao kila yanapotokea; hata kama huamini utaathirika vibaya na unyanyasaji huo. Kuripoti kunasaidia chumba cha habari kuelewa ukubwa wa tatizo na kuunda hatua muhimu za kukabiliana na tatizo hilo.

## Kuhusu IPI

Likiwa limeanzishwa mwaka 1950, shirika la International Press Institute (IPI) ni mtandao wa kimataifa wa wahariri, waandishi wa habari na wakuu wa vyombo vya habari ambao wamejitoa kwa pamoja kuhakika uwepo wa uandishi wa habari wa bora na ulio huru. Pamoja, tunakuza mazingira yanayowezesha uandishi wa habari kutekeleza jukumu lake kwa umma, ambalo muhimu zaidi ni uwezo wa vyombo vya habari kufanya kazi bila kuingiliwa na bila hofu ya kuadhibiwa. Dhamira yetu ni kutetea uhuru wa vyombo vya habari na mtiririko huru wa habari popote vinapokuwa hatarini.

## Kuhusu program ya Newsrooms Ontheline ya IPI programme

Lengo la programu ya Newsrooms Ontheline ya IPI ni kukusanya na kusambaza rasilimali na mbinu bora kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari ili kuzuia, kupambana na kushughulikia unyanyasaji na unyanyapaa wa mtandaoni dhidi yao. Kwa kutoa zana hizi kwa vyumba vya habari, inalenga sio tu kupambana na athari mbaya za kibinafsi na kitaaluma za unyanyasaji wa mtandaoni kwa waandishi wa habari, bali pia kusaidia kuzuia kujiziba mdomo kunakosababishwa na mashambulizi ya mtandaoni ambayo yanatishia upatikanaji wa habari kwa umma.

***Utengenezaji wa Mwongozo huu umewezeshwa na msaada wa kifedha wa Adessium Founda tion na Democracy & Media Foundation.***

***Hakimiliki:*** *Itifaki hii kwa vyumba vya habari kusaidia waandishi wa habari wanaolengwa na unyanyasaji wa mtandaoni imesajiliwa chini ya Leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution. Una uhuru wa kutumia tena Mwongozo huu alimradi tu unawataja waandaaji wa mwongo huu kwa ufasaha.*

# Mwongozo kwa vyombo vya habari wa kuwasaidia waandishi wanaolengwa na unyanyasaji wa mtandaoni

Kimataifa ya Creative Commons Attribution. Una uhuru wa kutumia tena Mwongozo huu alimradi tu unawataja waandaaji wa mwongo huu kwa ufasaha

**Mchapishaji**
International Press Institute (IPI)
*Februari 2020*

International Press Institute

Simu: + 43 1 512 90 11
Barua pepe: info@ipi.media
Tovuti: ipi.media

*The translation of this resource was coordinated by the IPI Africa program, with the support of the Government of Canada's Office of Human Rights, Freedoms and Inclusion (OHRFI).*

MWONGOZO WA KUPAMBANA NA UNYANYASAJI WA KIMTANDAO